# Twende Pamoja

HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

Hutolewa kila baada ya miezi Sita | Januari-June 2016 | Toleo Na 005

**Ndani**



Halmashauri ya wilaya yazindua soko la ununuzi wa mahindi Uk ......07

Shule ya wasichana ya Manyunyu yaongoza Mtihani wa Kidato cha Sita Mkoa wa Njombe. uk 10.



Habari katika picha Uk.11&12

# Halmashauri ya Wilaya ya Njombe yaongoza Kitaifa katika Usafi wa Mazingira.

*Uk 04.*







*Wafanyakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wakishangilia kwa furaha baada ya kutangazwa kuwa washindi wa kwanza kitaifa katika usafi wa mazingira. Mbali ya kupata zawadi ya gari linaloonekana nyuma ya picha pia walipata pikipiki katika sherehe zilizofanyika jijini Dar es Salaam.*

## Miradi ya zaidi ya shilingi Bilioni Moja yapitiwa na Mwenge Mwaka 2016 Wilayani Njombe.



*Kongozi wa mbio za mwenge Kitaifa akiwa na wakimbiza mwenge Wilayani Njombe..*

Jumla ya miradi 13 yenye thamani ya zaidi ya Sh. Bilioni moja imepitiwa na Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2016 ambao umekimbizwa kwa pamoja baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe na Mji Makambako wilayani Njombe.

*uk 4*

## Serikali yatuma Milioni 227 kwa ajili ya elimumsingi Njombe ......6



# Tahariri

Karibuni wasomaji wetu katika toleo lingine la *Twende Pamoja* ambalo ni gazeti linalomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe . Jarida hili hutolewa Kila baada ya miezi mitatu .

Dhima ya jarida hili mbali na kuhabarisha wananchi juu ya shughuli mbalimbali ambazo zinafanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa kipindi cha miezi mitatu mitatu pia ni kuwa nyenzo na daraja la kukuza maarifa na maendeleo katika Halmashauri .

Lengo la Halmashauri ni kuhakikisha Jarida la *Twende Pamoja* linapatikana katika kila Ofisi ya Kijiji na Kata ili kuwapa nafasi wananchi kusoma na kuelewa namna Halmashauri inavyotekeleza shughuli zake.

Tunaahidi kuendelea kutoa habari na makala ambazo zitakufanya uelewe namna sera zinavyotungwa, mipango inavyowekwa pamoja na utekelezaji wake unavyofanyika.

Tunatarajia matoleo yajayo yawe yamesheheni makala zenye kuelimisha na kuchochea maendeleo ya mtu mmoja mmoja, Kaya na Jamii kwa ujumla. Hii itakuwa nafasi nyingine ya kipekee ya kuweza kupata ujuzi na maarifa pasipo kuhitaji gharama.

Aidha tunakaribisha habari na makala mbalimbali kutoka kwenye Vijiji na Kata. Makala hizo zinaweza kuelezea jinsi utekelezaji wa miradi na shughuli mbalimbali za maendeleo zilivyofanyika katika Kijiji au Kata husika.

Tunakaribisha maoni na ushauri wa namna ya kuliboresha jarida hili kuweza kutimiza lengo la Halmashauri la kufanya kazi kwa uwazi na uwajibikaji. Tunawatakia usomaji mzuri. Sasa "Twende Pamoja.

Linatolewa na Ofisi ya

Mkurugenzi Mtendaji,

Halmashauri ya Wilaya

Njombe.

S.L.P 547 Njombe.

Phone: 026 2782111

Fax: 026 2782857

Email:ded@njombedc.go.tz

info@njombedc.go.tz

njombedc@yahoo.com

Tovuti:www.njombedc.go.tz

## Halmashauri yapata Mkurugenzi Mpya

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imepata Mkurugenzi mpya baada ya Rais John Pombe Magufuli kufanya uteuzi wa wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Miji, manisapaa na Majiji hivi karibuni.

Kufuatia uteuzi huo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe sasa itaongozwa na Bi Monica Peter Kwiluhya ambaye awali alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Same mkoani Kilimanjaro.

Awali Halmashauri ya Wilaya ilikuwa inaongozwa na Bi Hajjat Farida Mwasumilwe.

Bi Kwiluhya anakuwa Mkurugenzi wa 10 kuiongoza Halmashauri ya Wilaya ya Njombe tangu mwaka 1984 na kuwa mwanamke wa pili kuiongoza Halmashauri hii kama Mkurugenzi tangu mwaka huo.

Mkurugenzi anayeshikiria rekodi ya kuongoza Halmashauri hii kwa kipindi kirefu ni Bw. Mohamed Juma Mkupete ambaye aliongoza kwa kipindi cha miaka 7 kuanzia mwaka 2006 hadi 2012 alipomwachia Bw Paulo S Malala.



*Bi Monika Peter Kwiluhya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya wilaya ya Njombe.*

## Ujumbe wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Mwaka huu unasema “Vijana ni nguvu kazi ya Taifa” chini ya kauli mbiu inayosema “Washirikishwe nakuwezeshwa”.



# Miradi yenye thamini ya Bilioni 1 yapitiwa na Mwenge wa Uhuru Njombe.

Jumla ya miradi 13 yenye thamani ya zaidi ya Sh. Bilioni 1 imepitiwa na Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2016 ambao umekimbizwa kwa pamoja baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe na Mji Makambako wilayani Njombe.

Katika mwenge huu ambao umekimbizwa June 18, 2016 jumla ya Miradi 6 yenye thamani ya Tshs. 711,029,000 imewekewa Mawe ya Msingi, miradi 4 yenye thamani ya Tshs. 356,502,000 imefunguliwa na miradi 2 yenye thamani ya Tshs 147,188,650 imezinduliwa.

Sambamba na hilo miradi 3 yenye thamani ya Sh. 1.6 bilioni imekaguliwa na ugawaji wa hundi zenye thamani ya milioni 10 umefanyika kwa vikundi 6 vya vijana na 14 vya wanawake.

Aidha michango ya jamii katika miradi iliyopitiwa na mwenge mwaka huu ni shilingi milioni 420,561,100.

Ujumbe wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Mwaka huu unasema “Vijana ni nguvu kazi ya Taifa” chini ya kauli mbiu inayosema “Washirikishwe na kuwezeshwa”.

Katika kutekeleza ujumbe huu, Halmashauri ya wilaya ya Njombe na Mji Makambako zimekuwa zikiwashirikisha vijana katika uandaaji wa mipango hususani uibuaji wa miradi mbalimbali inayoweza kuwaongeza kipato na kuimarisha uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Aidha, Katika mwaka 2014/2015, Halmashauri zawilaya ya njombe na Mji Makambako zilitoa kiasi cha Tshs. 15,000,000.00 kati ya Tshs. Milioni 83,709,925.00 zilizotengwa ikiwa ni mikopo ya vikundi vya vijana 18 vyenye jumla ya wananchama 90 ili kukuza maendeleo yao binafsi na Taifa kwa Ujumla.

Mwaka huu wa 2015/2016, Halmashauri zimefanikiwa kutoa kiasi cha Tsh 21,000,000 kati ya Tshs. 138,775,865.00 ikiwa ni mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi vya vijana vipatavyo 21 vyenye jumla ya wanachama 105 kwa ajili ya kukuza maendeleo yao binafsi na Taifa kwa ujumla.

Sambamba na ujumbe mkuu pia mwenge wa uhuru mwaka 2016 uliambatana na ujumbe kuhusu Mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI, mapambano dhidi ya Malaria, mapambano dhidi ya matumizi ya Dawa za kulevya pamoja na mapambano dhidi ya Rushwa.

Katika Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2015 jumla ya Miradi 10 yenye thamani ya Shilingi 3,556,570,678.55 ilipitiwa na Mbio za Mwenge wa Uhuru. Miradi hii ilitekelezwa kwa kushirikisha Wahisani, Serikali kuu, Halmashauri na nguvu za wananchi.

# Milioni 227 zatumika kuendesha elimu bure shule za Sekondari Njombe.

Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais John Pombe Magufuri imetekeleza kwa vitendo ahadi ya kutoa elimu bure kwa elimu ya msingi na sekondari baada ya kuipatia Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kiasi cha Sh.227 milioni kwa ajili ya kuendesha shule za msingi na sekondari wilayani hapa.

Fedha hizo ambazo zimetumika kuendeshea shughuli mbalimbali katika shule 10 za Sekondari na shule 52 za msingi zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ni za kipindi cha miezi sita kuanzia mwezi Desember 2015 hadi Mei 2016.

Shughuli zilizofanyika ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ukarabati wa miundombinu ya shule ikiwemo majengo, mifumo ya maji, umemena samani.

Matumizi mengine ni pamoja na uendeshaji wa mitihani endelezi, uendeshaji wa michezo pamoja na kazi za utawala.

Upande wa elimu ya sekondari hadi kufikia mwezi mei mwaka huu serikali ilituma Tsh 159 milioni kwa ajili ya kutumika kwenye shule 10 za serikali za sekondari zilizopo katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe.

Aidha upande wa shule za msingi kwa kipindi cha mwezi desemba 2015 hadi mei 2016 serikali imetuma shilingi 67 milioni kwa ajili ya kutumika kwenye shule 52 za msingi za serikali zilizoko katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe.

Katika kuhakikisha fedha zinazotolewa na serikali zinatumika kama ilivyokusudiwa Halmashauri ya wilaya ya Njombe tayari ilishasambaza miongozo mbalimbali ya matumizi ya fedha ya ruzuku ya uendeshaji shule.

Sambamba na hilo halmashauri imetoa imetoa mafunzo katika Nyanja za manunuzi, uhifadhi wa vifaa vya kielimu vinavyonunuliwa pamaoja na ukaguzi.

Pamoja na nia nzuri na thabiti ya serikali ya kuhakikisha uwepo wa fursa ya elimu bora kwa wote na kuwapunguzia mzigo wazazi,walezi kugharamia ,kuchangia elimumsingi katika shule za serikali lakini bado wajibu wa mzazi umebaki palepale.

Wajibu ho ni pamoaja na kuhakikisha wanafunzi wanakuwa na sare za shule na michezo, vifaa vya kujifunzia vikiwemo daftari na kalamu, chakula kwa wanafunzi wa kutwa, matibabu, nauli ya kwenda na kurudi kwa wanaotumia usafiri na walioko shule za sekondari za bweni wakati wa likizo pamoja na mahitaji mengine ya kibinadamu kwa wasichana na wavulana kama vile magodoro, shuka na mito.

# Wenyeviti wa Serikali za vijiji wapewa mafunzo.

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe katika kuimarisha dhana ya utawala bora imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kuboresha utendaji wa kazi wenyeviti wa serikali za vijiji wilayani hapa.

Mafunzo hayo yametolewa kwa wenyeviti wa serikali za vijiji 45 kutoka katika vijiji 45 vilivyopo katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe ambao waliingia madarakani mwaka 2014.

Mafunzo hayo yaliyofunguliwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Bi Hajjat Farida Mwasumilwe, pamoja na kuwajengea uwezo kwenye dhana ya utawala bora pia yalilenga kuwapatia mbinu mbalimbali za masuala uongozi.

Maeneo mengine waliojengewa uwezo ni dhana ya rushwa katika jamii, majukumu na muundo wa serikali za kitongoji na kijiji pamoja na mafunzo juu ya kufanya tathimini na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maneo yao.

Akifungua mafunzo hayo Mkurugenzi Mwasumilwe aliwataka wenyeviti wa vijiji kufanya kazi vizuri pamoja na kupunguza migogoro baina ya wananchi na watendaji, watendaji wa vijiji na wenyeviti wa vijiji sambamba na kupunguza na kutatua migogoro ya ardhi katika maeneo yao.

“Ni jukumu lenu kusaidia ukusanyaji wa mapato kwa kuwa nyinyi ndio wenye watu, lazima kuzingatia matumizi bora ya ardhi ikiwemo suala la usafi wa mazingira katika maeneo mnayoishi” alisema Hajjat Mwasumilwe.

“Hakikisheni mnatoa elimu kwa wananchi juu ya lishe na kuwataka wananchi wawekeze kwenye elimu pamoja na kuwapa watoto lishe ya kutosha badala ya kuwekeza kwenye pombe, tukiwekeza kwenye elimu na lishe tutajenga taifa bora na imara.” Alisisitiza Hajjat Mwasumilwe.

Aliwasisitiza kusimamia ujenzi wa miundo ikiwemo suala la madawati kwa shule za Msingi huku wakikubaliana kufanya tathimini ya maagizo waliyopewa mwezi wa nane mwaka huu.

# Halmashauri ya Njombe yaongoza Kitaifa Usafi wa Mazingira

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imeibuka kuwa mshindi wa Jumla wa usafi wa mazingira katika mashindano ya afya na usafi wa mazingira mwaka huu.

na kuifuta historia ya usafi wa mazingira Halmashari ya Moshi kwa kushika.

Halmashauri ya Njombe imepata asilimia 97 ya usafi wa mazingira na kufuatia Halmashauri ya Iringa Mjini kwa asilimia 81.1.Kufuatia ushindi huu Halmashauri ya wilaya ya Njombe imefanikiwa kipiku Halmashauri ya Moshi ambayo imekuwa ikiibuka na ushindi wa jumla kwa kipindi kirefu.

Akizungumza wakati wa kutoa tuzo kwa Halmashauri ,Manispaa, Majiji, Miji pamoja na Vijiji ,Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu amesema kuwa Halmashauri ya Njombe haijaripoti mgonjwa wa kipindupindu hata mmoja tangu ugonjwa huo ulipotiwe Agasti mwaka jana.

Amesema kuwa Halmashauri ya wilaya ya Njombe imeweza kuwa na vyoo bora kwa asilimia 95 katika vijiji yake pamoja na kuwa vifaa vya kunawia mikono katika vyoo hivyo.

Kufuatia ushindi huo Halmashauri wilaya ya Njombe imepata tuzo ya gari aina ya Land Cruiser Hardtop, Kombe, Cheti, pamoja na pikipiki katika vijiji vitatu ambavyo vimefanya vizuri katika suala la usafi wa mazingira.

Sambamba na hilo Halmashauri ya wilaya ya Njombe imeweza kushika nafasi tatu za juu kwa upande wa vijiji vilivyotekeleza vizuri kampeni hii. Nafasi ya kwanza kitaifa imeshikwa na kijiji cha Wanginyi Kata ya Matembwe , nafasi ya pili imeshikwa na kijiji cha Matiganjola huku nafasi ya tatu ikishikwa na kijiji cha Sovi Kata ya Mtwango.

Upande wa majiji Mbeya wameibuka na ushindi wa kwanza katika majiji kati ya majiji manne kutokana na kufanya usafi wa mazingira kwa kuweka mifumo ya uhifadhi takataka.

Kufuatia ushindi huo jijila mbeya limepata tuzo kikombe ,pikipiki pamoja na cheti huku Halmshauri ya Mji mdogo wa Tunduma nao ukiibuka kuwa mshindi wa usafi wa mazingira kwa upande wa miji.

Halmashauri zingine zilizopa tuzo hizo ni pamoja na Kahama,Mpanda ,Kondoa ya Kinondoni ambapo zimetunikiwa tuzo ya vikombe, pikipiki pamoja na vyeti.

Kwa upande wa Hospitali za Rufaa iliyoongoza ni Mount Meru ikifuatia na Hospitali ya Amani katika nafasi ya pili huku Hospitali ya Morogoro ikishika nafasi ya tatu.






*Picha kushoto wafanyakazi wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe wakishangilia baada ya kutangazwa kuwa washindi wa kwanza kwenye usafi wa mazingira na kupewa zawadi ya gari jijini dar es salaama. Picha kulia viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Njombe wakiwa pamoja na wafanyakazi wa Halmashauri ya wilaya pamoja na wenyeviti wa serikali za vijiji katika picha ya pamoja baada ya kukabidhiwa zawadi na Mkuu wa mkoa wa Njombe Dr Rehema Nchimbi.*

# Wakulima wa mbogamboga na matunda kunufaika Njombe.



*Mafundi wakiendelea na ukarabati wa kituo cha kuzuia upotevu wa mazao na mbogamboga ambacho kitasaidia kuzuia upotevu wa mazao na kuinua kipato cha mkulima Mkoani Njombe.*

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kupitia programu wa MIVARF wanakarabati kituo cha mafunzo ya kuzuia upotevu wa mazao ya mboga mboga na matunda katika eneo la makao makuu ya Halmashauri Njombe Mjini.

Lengo la mradi huu ni kuwawezesha wakulima wa mazao ya mbogamboga na matunda (Horticultural crops) kuzuia upotevu na kuongeza thamani ya mazao ili kumuongezea mkulima kipato.

Kupatikana kwa mradi huu kunatokana na jitihada za Halmashauri ya wilaya ya Njombe katika kuandaa maandiko mbalimbali ya uwekezaji wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kusaidia wananchi na kuongeza mapato ya Halmashauri.

Mradi huu ambao unafadhiliwa na programu Mivarf ni muendelezo wa mradi mwingine wa kuimarisha zao la mnyororo wa mahindi unaofadhiliwa na MIVARAF kupitia taasisi ya Uongozi na Maendeleo ya Ujasiliamali ambao unatekekezwa katika vijiji13 kwenye kata za Ninga, Ikuna, na Kichiwa wilayani Njombe.

Kazi kubwa inayofanywa na MIVARF kwa kushirikiana na Halmashauri ya wilaya ya Njombe ni kuwajengea uwezo wakulima na vikundi vya uzalishaji ikiwemo AMCOS na kuwaunganisha wakulima na masoko kwa zao la mnyororo wa thamani lililochaguliwa ambalo ni mahindi.

Ukarabati wa kituo hiki utaghalimu zaidi ya Tsh 74 milioni na unatekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza inahusisha ukarabati na awamu ya pili usimikaji wa mitambo.

Upande wa ukarabati hadi sasa uko kwenye hatua za ukamilishaji huku usimikaji wa mitambo ukiwa kwenye mchakato wa manunuzi.

Ukarabati ukikamilika kituo kitakuwa kinuwezo wa kuchukua watu 40 kwa wakati mmoja na kitahudumia wakulima wa Mkoa wa Njombe ambao ni wazalishaji wa mazao ya matunda na mbogamboga hususani zao la nyanya ambalo linalimwa kwa wingi Mkoani Njombe.

Uwepo wa kituo hiki unatoa fursa kwa vikundi kuweza kupata mafunzo ya stadi za usindikaji wa mazao jambo litakalosaidia kupunguza upotevu wa mazao na kuongeza thamani na kipato.

# Huduma za afya zaanza kutolewa Vijiji matiganjola na Ibiki.

Katika kuboresha huduma za afya kwenye jamii Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kupitia Idara ya afya imeanzisha huduma za zahanati katika vijiji vya Matiganjola Kata ya Ikuna na Ibiki kata ya Igongolo wilayani hapa.

Kuanzishwa kwa huduma hizi kunafuatia kazi kubwa iliyofanywa na jamii ya kukarabati majengo na kutafuta nyumba za watumishi ambapo Halmashauri ilifanya ukaguzi na kujiridhisha kuwa zinaweza kuanza kutoa huduma ya afya huku mikakati ya ujenzi ikiendelea.

Tayari Halmashauri imechukua jukumu la kununua dawa ili huduma iendelee kutolewa katika zahanati hizo wakati maombi ya kibali cha dawa kwa ajili ya vituo hivi ili kupata ruzuku ya mgao wa dawa kama zahanati zingine za kiserikali yakisubiliwa kujibiwa. Sambamba na hilo tayari watumishi watatu wamepelekwa katika zahanati ya Matiganjola ambao ni afisa tabibu, muuguzi na mhudumu wa afya. Upande wa Ibiki tayari amepelekwa tabibu msaidizi na muuguzi yupo katika hatua ya kupelekwa.

Katika zahanati hizo huduma zimeanza kwa wagonjwa wa n je na huduma zingine zitaendelea kuongezwa mara baada ya kupata vifaa ikiwemo friji za kuhifadhia dawa na vitanda kwa ajili ya kuzalishia.

# Wanafunzi 612 wafanya mtihani wa kidato cha nne Njombe.

Jumla ya wanafunzi 612 wamefanya mtihani wa kumaliza kidato cha nne kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.
Katika mitihani hiyo iliyofanyika mwezi Novemba mwaka huu, Wasichana waliofanya mtihani walikuwa 398 na wavulana 214ambao ni sawa na asilimia 98.55 huku wanafunzi ambao hawakufanya mtihani wakiwa ni 11 wasichana wakiwa 7 na wavulana 4.

Wanafunzi waliofanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne mwaka huu ni wale walioandikishwa kuingia kidato cha kwanza mwaka 2012. Mwaka 2012 wanafunzi walioandikishwa kuingia kidato cha kwanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe walikuwa 1645 wasichana wakiwa 927 na wavulana 715.

Aidha, kati ya wafunzi 1645 walioandikishwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2012 wanafunzi 505 hawakufika kidato cha nne mwaka 2015 kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo utoro, ugonjwa, vifo pamoja na kukariri darasa kutoka na kufeli mtihani wa kidato cha pili.

Katika wanafunzi 505 walioshindwa kumaliza mtihani wa kidato cha nne mwaka huu wasichana ni 329 na wavulana ni 176 na hakuna mwanafunzi yoyote aliyeshindwa kumaliza mtihani ya kidato cha nne kutokana na mimba.

Ili kuhakikisha idadi ya wanafunzi wanaokariri madarasa inapungua Halmashauri ya wilaya ya Njombe kupitia Idara ya Elimu ya Sekondari imeweka mikakati mbalimbali kufanikisha suala hilo.

Mikakati hiyo ni pamoja na Kuhakikisha shule zinatoa chakula cha mchana ili kuwapa wanafunzi muda mwingi wa kujifunza, kuwapa masomo rekebishi pamoja na kuwapa ushauri ili kuwajengea mazingira mazuri ya kijifunza.

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe inajumla ya Shule 12 ambapo jumla ya Shule 10 zilifanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne mwaka huu na mtihani huo umefanyika kwa njia ya amani na utulivu na hakukuwa na tukio lolote la udanganyifu lililotokea.



*Wanafunzi wa shule ya Sekondari Sovi wakiwa katika mafunzo kwa vitendo kabla ya mtihani wa Taifa*

# TANGAZO

Halmashauri ya wilaya ya Njombe imefanya marekebisho ya sheria ndogo zinazohusu Ada na ushuru wa mazao, bidhaa na huduma mbalimbali ambapo sheria ndogo hizo zimeshatolewa katika gazeti la Serikali kwa **Tangazo la serikali Na. 471 la 23.10.2015.**

Kwa mujibu wa tangazo la serikali Na 471 (2015)

i. Kila msafilishaji wa mazao ya misitu atatakiwa kulipa tozo asilimia ishirini (20%) juu ya ada ya usafirishaji (Transist Pass-TP) wa mazao ya misitu. Kwa tafsiri hiyo,

| S/Na | Ujazo wamzigo katika Gari | Tozo la 20 Halmashauri(HW5) |
|---|---|---|
| 1 | Zaidi ya Tani 7 | 3000/= |
| 2 | Chini ya Tani 7 | 1500/= |

ii. Kila mfanyabiashara wa mazao ya misitu atatakiwa kulipa tozo ya asilimia kumi (10) juu ya ada ya Usajili ya wafanyabiashara wa Mazao ya Misitu na wenye Viwanda vya kuchakata mazao ya misitu . Viwango vya tozo hizi vimeambatanishwa hapa chini. Tozo hii haitawahusu wafanyabiashara wa mazao ya misitu waliokwisha sajiriwa kabla ya Tangazo la Serikali Na 471 la Octoba 23,2015

Tozo hizi zitawahusu wafanyabiashara wote wanaofanyia kazi katika eneo la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

**Atakayekiuka agizo hili atatozwa faini ya kiasi cha shilingi elfu hamsini (Tsh 50,000) na Au kifungo cha miezi kumi na mbili(12)**

MCHANGANUO WA VIWANGO VYA TOZO ZA ADA YA USAJILI WA WAFANYABIASHARA WANAOJISHUGHULISHA NA UCHAKATAJI AU BIASHARA YA MAZAO YA MAZAO YA MISITU KWA ENEO HUSIKA KWA KILA MWAKA.

| S/Na | AINA YA ZAO LA MISITU/ BIASHARA | ADA YA HATI YA USAJILI (REGISTRATION) INAYOLIPWA SERIKALI KUU (ERV) TSHS | TOZO LA 10% LA ADA YA USAJILI (TSHS) HW5 INALIPWA HALMASHAURI. |
|---|---|---|---|
| 1 | Biashara ya Mbao (Timber) | 256,000 | 25,600 |
| 2 | Biashara ya Magogo (Logs) | 256,000 | 25,600 |
| 3 | Biashara ya Nguzo (Poles) | 256,000 | 25,600 |
| 4 | Biashara ya Miti (Trees) | 270,000 | 27,000 |
| 5 | mashine za kuchana Mbao (Sawmill) 5000m3 per year | 512,000 | 51,000 |
| 6 | Mashine za kuchana Mbao (sawmill) 5001-10,000m3 per year | 1,000,000 | 100,000 |
| 7 | Kiwanda cha kutengeneza Chipboard (ChipboardMill) | 1,000,000 | 100,000 |
| 8 | Kiwanda cha kutengeneza Hardboard (Hardboard Mill) | 1,000,000 | 100,000 |
| 9 | Kiwanda cha kutengeneza Plywood (Plywood mill) | 1,000,000 | 100,000 |
| 10 | Kiwanda cha kutengeneza Karatasi | 2,000,000 | 200,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11 | Kiwanda cha kutengeneza Viberiti (Match Box Factory) | 1,000,000 | 100,000 |
| 12 | Kiwanda cha kutibu Mazao ya Misitu (Nguzo,Mbao nk) Impregnation Plant | 512,000 | 51,200 |
| 13 | Duka la Vinyago na Mapambo yatokanayo na Mazao ya Misitu (Curio Shops-Forestry Products) | 256,000 | 25,600 |
| 14 | Watoaji wa mazao ya Misitu nje ( Exporters of Forestry Products) | 512,000 | 51,200 |
| 15 | Waingizaji wa mazao ya Misitu ndani ya Nchi (Importers of Forestry Products) | 512,200 | 51,200 |
| 16 | Biashara ya Mkaa (Charcoal) | 256,000 | 51,200 |
| 17 | Biashara ya Kuni (Firewood) | 256,000 | 51,200 |
| 18 | Duka la Samani ( Furniture Mart) Kubwa | 256,000 | 51,200 |
| 19 | Duka la Samani (Furniture Mart ) Ndogo | 256,000 | 51,200 |
| 20 | Kiwanda cha kuchakata Miti au Mbao (Wood Works Factory) Mashine za kukereza n.k Kubwa | 384,000 | 38,400 |
| 21 | Kiwanda cha kuchakata miti au mbao (Wood Works Factory) Mashine za Kukereza n.k Ndogo | 150,000 | 15,000 |
| 22 | Fundi Seremala (Carpentry) | 50,000 | 15,000 |
| 23 | Biashara ya mazao mengine ya Misitu | 130,000 | 13,000 |

**N:B Utekelezaji wa Agizo hili unaanza mara moja.**

Limetolewa na
Hajjat Farida A Mwasumwilwe
**Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.**

## KUTOKA MAKTABA





*Kushoto wataalamu wa Halmashauri na madiwani wakikagua ujenzi wakikagua chanzo cha maji katika mradi wa maji kijiji cha Ihangana na Kulia waziri mkuu wa zamani Mh Mizengo Pinda akikagua shamba la mananasi katika kijiji cha madeke alipofanya ziara katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.*

# Manyunyu Sekondari yaongoza kwa ufaulu mitihani ya Kidato cha Sita Mkoa wa Njombe

Shule ya Sekondari ya wasichana ya Manyunyu iliyoko Kata ya Mtembwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imeshika nafasi ya kwanza Mkoa wa Njombe katika matokeo ya mtihani wa kidato cha sita mwaka 2016.

Sekondari ya Manyanyu imeshika nafasi ya kwanza kati ya shule 11 za sekondari zilizofanya mtihani wa kidato cha sita mkoani Njombe huku kitaifa ikishika nafasi ya 41 kati ya shule 423.

Katika matokeo yaliyotangazwa na baraza la mitihani hivi karibuni jumla ya watahiniwa 136 walifanya mtihani huo kutoka shule ya sekondari ya Manyunyu na kufauli katika kiwango cha daraja la kwanza hadi la tatu.

Kwenye matokeo hayo wasichana waliopata daraja la kwanza wako 30 daraja la pili wako 83 na daraja la tatu wako 23 huku kiwango cha ufaulu kikiwa ni asilimia 100.

Nayo Shule ya Sekondari ya Mtwango inayopatikana katika Kata ya Mtwango wilayani Njombe imeshika nafasi ya 3 kimkoa kati ya shule 4 ambazo zinawanafunzi pungufu ya 30 na kitaifa imeshika nafasi ya 76 kati ya shule 117.

Mwaka huu jumla ya wanafunzi 200 wamechanguliwa kujiunga na elimu ya kidato cha tano katika shule ya wasichana ya Manyunyu ambayo inamchepuo wa masomo ya sanaa na sayansi.

Akizungumzia sababu zilizopelekea shule ya Sekondari ya Manyunyu kufanya vizuri afisa elimu taaluma wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Bw. Christopher Haule alizitaja sababu hizo kuwa ni usimamizi mzuri, hali na bidii ya walimu katika kufundisha Pamoja na mazingira rafiki ya kufundisha na kujifunzia wanafunzi shuleni hapo.

Kwa upande wake mkuu wa shule ya Sekondari ya Manyunyu Bi Neema Nzoa alisema kuwa sababu zilizopelekea shule ya Manyunyu kufanya vizuri ni pamoja na ushirikiano uliopo baina ya uongozi wa shule na walimu pamoja na wanafunzi ambao wamekuwa wepesi kutoa taarifa pindi wanapopatwa na shida.

“ Tumekuwa na utaratibu wa kuongea na kuwashauri wanafunzi ili kuweza kufahamu matatizo yao na kisha kuwashauri, Mitihani inapotungwa huwa inapitiwa na idara husika kisha walimu wa taaluma, matokeo yanapotoka tunayapitia kwa pamoja na ikitokea kuna soma wanafunzi wamefanya vibaya mwalimu husika anaitwa na kuulizwa imekuwaje kisha tunamshauri” alisema Bi Nzoa.

Aliongeza kuwa wanafunzi wa Shule ya Manyunyu wamekuwa na utamaduni wa kutafuta mitihani kutoka Shule zingine na kuifanya ambapo walimu wamekuwa wakitoa misaada ambayo imekuwa ikisaidia kuinua kiwango cha taaluma Shuleni hapo.

## HABARI KWA UFUPI.

*Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ina jumla ya miradi 65 ya maji inayotumia teknolojia mbalimbali katika kutoa huduma ya maji safi na salama. Miradi inayotumia teknolojia ya maji mtiririko ipo 11, inayotumia mashine ya dizel ipo 4, na inayotumia nishati ya umeme ipo 4.*

*Miradi mingine 7 inatumia hydram (hydraulic ram) inayosukumwa na nguvu ya maji, miradi mitata (3) inayosukumwa na nguvu ya maji kwa kutumia magurudumu ijulikanayo kama water wheel, mradi wa nishati ya jua (solar) upo mmoja.*

*Aidha halmashauri ya wilaya ya njombe ina visima vifupi 35 na visima virefu 2. Kutokana na uwepo wa miradi hii jumla ya watu 45,735 kati ya watu 85,747 sawa na asilimia 53.3 ya wananchi waliopo katika halmashauri ya wilaya ya njombe wanapata maji safi na salama.*





*Picha juu Mbunge wa jimbo la Lupembe Jolam Hongoli akiangalia tank la kuhifadhia maji kijiji cha Ukalawa.Miundo mbinu ya Uvunaji wa maji ya mvua shule ya msingi Ihang’ana*



*Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe Bw Valentino Hongoli akipampu maji katika shule ya Msingi Kidegembye wakati wa ukaguzi wa miradi* maendeleo.



*Madiwani pamoja na wataalamu wa Halmashauri ya Wilaya Njombe wakiangalia chanzo cha maji katika mradi wa maji Kijiji cha Ukalawa .Mradi huu utahudumia vijiji viwili vya Ukalawa na Kitole.*



*Mhandisi wa Ujenzi Halmashauri ya wilaya ya Njombe Bw. Samson Kalesi (kushoto) akitoa maelezo juu ya ujenzi wa barabara ya Ninga -Kichiwa kwa madiwani wa Halmashauri ya Wilaya wakati wa ukaguzi wa miradi ya maendeleo.*



*Walimu wa shule za Msingi wakimsikiliza afisa manunuzi wakati akitoa semina juu ya masuala ya manunuzi kupitia mpango wa elimumsingi bure ambapo walipewa semina kuhusu utunzanji wa fedha, manunuzi na ukaguzi.*



*Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wakipima upana wa barabara ya Kichiwa wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Halmashauri ya wilaya ya Njombe kwa mwaka wa fedha 2015/2016*



*Moja ya maghala ya kuhifadhiwa mazao ambalo limekarabatiwa na Wizara ya Kilimo kupitia mpango wa kutekeleza kwa matokeo makubwa (BRN). Pichani ni ghala la kuhifadhia mazao katika Kijiji Ukalawa linahifadhi tani 300 za chakula.*



*Kaimu Mkuu wa wilaya ya Njombe (wakati huo) Bw Anatoli Choya akitoa melezo mbele ya kiongozi wa mbio zamwenge wa Uhuru Ndg, George J Mbijima katika moja ya miradi ya maendeleo iliyopitiwa na mwenge mwaka 2016.*



*Wafanyakazi wa TANROAD Njombe ni miongoni mwa wadau walioitikia uchangiaji wa madawati. Pichani wakiwa mbele ya madawati waliyochangia katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.*



*Mkurugenzi Mtendaji wa zamani wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Bi Hajjat Farida Mwasumilwe akizungumza na walimu wa shule za Msingi katika moja ya ziara zake za kusikiliza kero pamoja na kutoa maelekezo mbalimali ya Serikali kwa watumishi wa wa Halmashauri .*



*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Valentino Hongori akinyanyua kombe ambalo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imekabidhiwa baada ya kuibuka mshindi katika usafi wa mazingira.*



*Moja ya ubunifu katika Shule ya Msingi Kidegembye ambapo wametengeneza ramani ya Afrika kwa kutumia chupa za plastiki za maji na soda kwa ajili ya wanafunzi kujifunza .*



*Mkuu wa Wilaya ya Njombe Bi. Luth B. Msafiri akiwa ameshika cheti cha ushindi wa usafi wa mazingira mara baada ya kukabidhiwa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe Dr Rehema nchimbi. Kulia ni mwenyekiti wa wa Halmashauri ya Njombe Valentino Hongoli akiwa na kombe.*